

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOANA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

---

SHULE YA SEKONDARI UKUKWE,  
S.L.P 346,  
**TUKUYU.**

.....  
SIMU: 0766 240 768

0787 701 906

Kumb.Na.Ukk/ss/Vol.Na27/69

JINA LA MWANAFUNZI \_\_\_\_\_

S.L.P \_\_\_\_\_

RUNGWE.

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UKUKWE WILAYA YA RUNGWE MKOA WA MBEYA-2021.**

**0.1 UTANGULIZI**

Ninayofuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari UKUKWE ni ya serikali ,ipo kijiji cha ILOLO kata ya KIWIRA wilaya ya RUNGWE Mkao wa MBEYA .Shule itafunguliwa rasmi tarehe 11/01/2021 na mwisho wa usajili ni tarehe 18/01/2021 (ndani ya siku saba).

Napenda kukupongeza na kukumbusha kuwa nafasi hii uliyopewa ni bahati yako ambayo vijana wengine kama wewe wameikosa.Na ni matumaini yangu kuwa utatumia vema nafasi hii na mazingira ya shule ipasavyo kuijendeleza ili upate ELIMU inayokusudiwa kwa manufaa yako na Taifa pia.Itawezekana tu ukiwa na NIDHAMU,MAARIFA,UAMINIFU NA UADILIFU NDANI NA NJE YA SHULE.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE KWA WAVULANA**

- i. Suruali mbili (2) nyeusi (1) na kijivu (1)
- ii. Mashati mawili (2) meupe (tetroni) fupi mikono
- iii. Sweta la baridi moja(1) Rangi ya kijivu
- iv. Viatu Rangi nyeusi jozi (2) kisigino kifupi
- v. Soksi Rangi nyeupe jozi mbili (2)
- vi. Fulana (kaoshi) ya ndani Rangi Nyeupe.
- vii. Mikanda miwili (2) ya suluali rangi nyeusi isiyo na kibanio kikubwa.

**2.2 SARE ZA SHULE KWA WASICHANA**

- i. Sketi mbili ndefu kuzidi magoti zenyе marinda Rangi nyeusi (1) na kijivu (1).
- ii. Mashati mawili (2) rangi nyeupe (tetron) fupi mikono.
- iii. Sweta la baridi moja Rangi ya kijivu.
- iv. Viatu Rangi nyeusi jozi (2) kisigino kifupi.
- v. Fulana (kaoshi) ya ndani Rangi Nyeupe.
- vi. Soksi jozi mbili (02) rangi nyeupe ndefu saizi ya magoti.

vii. Hijabu kwa waislamu Rangi nyeupe isiyo na maua.

### **2.3 MAHITAJI YA DARASANI (VIFAA VYA KUJIFUNZIA KWA WOTE)**

- i. Daftari counter quire 3 au 4 kumi(10)
- ii. Mathematical set ( mkebe) mmoja (1)
- iii. Kalamu pencel na peni za kutosha
- iv. Kamusi (dictionary)
- v. Begi dogo la kubebaa madftari na vifaa vingine vya darasani.

### **2.4 SARE ZA MICHEZO (KWA WOTE)**

- i. T-shirt ya blue moja (01)
- ii. Traksuti rangi ya blue
- iii. viatu au raba jazi moja Rangi yoyote

### **2.5 VIFAA VYA USAFI**

- i. Kindoo kidogo cha plastiki lita 10.
- ii. Fyekeo (kwanja).

### **2.6 CHAKULA**

Mwanafunzi anatakiwa kupata chakula cha mchana awapo shulenii.Ni jukumu la mzazi kumpatia chakula mwanafunzi kwani ratiba ya masomo mwisho saa 11:00 jioni.Hata hivyo,namna ya kuchangia chakula ni kama itakavyoamuliwa kikao cha wazazi.

## **3.0 MAMBO MENGINE MUHIMU**

- i. Utatakiwa kujaza fomu ya “medical Examination” ambavyo utakabidhi pamoja na cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi mara utakaporipoti shule.
- ii. Utajaza fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki fujo,migomo,utoro shulenii na kukubaliana na sheria na kanuni za shule.

### **3.1 SHERIA NA KANUNI MUHIMU**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na .25 ya mwaka 1979 na iliyoboreshwaa kwa seria Na.10 mwaka 1995 Aidha inazingatia miongozo inayotolewa na Wizala ya Elimu,sayansi na Teknolojia yenye dhaman ya elimu chini ya ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo kama yalivyooleza

- A. Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote ,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazma.
- B. Mahuzurio mazuri katika sughuli za ndani na nje ya sole kulingana na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- C. Kushiriki kwa makini mandalio ya jioni(preparation).
- D. Kuwahi katika sughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- E. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- F. Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
- G. Kuvaa sale ya shule wakati wote unapotakiwa.
- H. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- I. Kutunza mali za uma

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.**

- a. Wizi.
- b. Uasherati na ushoga.
- c. Ubakaji.
- d. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi ,cocaine,kubeli na kudhalika.
- e. Kupigana na kupiga.
- f. Kuhalibu kwa makusudi mali ya umma.
- g. Kudharau bendela ya Taifa.
- h. Kuwa mjamzito/kupata mimba.
- i. Kuoau kuolewa.
- j. Kutoa mimba.
- k. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa sule au watu.
- l. Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m. Kuwa na simu ya mkononi.

Unatakiwa kusoma kwa makini maelezo yote katika fomu hii na kuyatekeleza kwa muda muafaka na endapo hutaelewa wasiliana na Uongozi wa shule kuitia namba za simu tajwa.

**KARIBU SANA UKUKWE SEKONDARI**

.....  
**ISAKWISA DB  
MKUU WA SHULE**